Siionei Haya Injili

(Not Ashamed Of The Gospel)

Na

Ellis P. Forsman

Siionei Haya Injili

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 7, 2011

Siionei Haya Injili

Rum. 1:14-17

Paulo anaanza waraka wake kwa Warumi, aliandika kuhusu hamu yake ya kutaka kuwaona.

Maombi yake ya bidii kwa mwisho huo. Rum. 1:9-10, "*Kwa maana Mungu nimwabuduye kwa roho yangu katika injili ya mwana wake, ni shahidi wangu jinsi niwatajavyo pasipo kukoma, siku zote katika sala zangu nikiomba nije kwenu hivi karibuni, Mungu akipenda kuifanikisha safari yangu.*"

Hamu yake katika kuwahimiza wapate elimu njema. Rum. 1:11-12, "*Kwa maana ninatamani sana kuwaona nipate kuwapa karama ya rohoni, ili mfanywe imara; yaani tufarijiane mimi na ninyi kila mtu kwa imani ya mwenzake, yenu na yangu.*"

Mipango yake ya kuja, ili aweze kupata matunda kutoka kwao. Rum. 1:13, "*Lakini ndugu zangu zipendi msiwe na habari ya kuwa mara nyingi nalikusudia kuja kwenu, nikazuiliwa hata sasa, ili nipate kuwa na matunda kwenu ninyi pia kama nilivyo nayo katika mataifa mengine.*"

Hamu yake ya kutaka kuwaona ilihusiana na injili, aliyoitunza kama mtume wa Kristo.

Rum. 1:1, "*Paulo mtumwa wa Kristo Yesu aliyeitwa kuwa mtume na kutengwa aihubiri injili ya Mungu.*"

Habari njema kuhusu Yesu. Rum. 1:3, "*Yaani habari za Mwanawe aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili.*"

Ambayo hakuionea haya. Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Je tunaionea haya injili ya Kristo? Unachukia kuwaambia wengine kuhusu Yesu? Je hii inaweza kuwa tatizo la wengi kutofanya vizuri katika uinjilisti binafsi?

Labda kwa kuchunguza namna na kwa nini Paulo hakuionea haya injili, tunaweza tukawa na juhudi zaidi katika kushiriki habari njema ya Yesu Kristo.

Paulo hakuionea haya injili

Jinsi ambavyo hakuona haya…

Ajisikia kuwa na wajibu wa kuhubiri injili kwa kila mtu.

Kwa Wayunani na wasio Wayunani wenye hekima na wasio na heki.

Rum. 1:14, "*Nawiwa na Wayunani na wasio Wayunani, nawiwa na wenye hekima na wasio na hekima.*"

Juhudi zake katika upendeleo ambao Mungu amemwonyesha.

- 1 Kor. 15:9-10, "*Maana mimi ni mdogo katika mitume, nisiyestahili kuitwa mitume, kwa sababu naliliudhi kanisa la Mungu. Lakini kwa neema ya Mungu nimekuwa hivi nilivyo, na neema yake iliyo kwangu ilikuwa si bure, bali nalizidi sana kufanya kazi kupita wao wote; wala si mimi bali ni neema ya Mungu pamoja nami.*"
- 1 Tim. 1:12-14, "*Nami namshukuru Kristo Yesu Bwana wetu, aliyetia nguvu kwa sababu aliniona kuwa mwaminifu akaniweka katika utumishi wake; ingawa hapo kwanza nalikuwa mtukanaji; mwenye kuudhi watu, mwenye jeuri, lakini nalipata rehema kwa kuwa nalitenda hivyo kwa ujinga na kwa kutokuwa na imani.*"

Alikuwa tayari kuhubiri injili katika Rumi.

Nafasi yoyote aliyopewa, angeweza kufanya vizuri! Rum. 1:15, K*adiri alivyo ndani yangu, niko tayari kuhubiri injili hata kwenu ninyi mlioko Rumi.*"

Hataivyo matakwa yake ilikuwaa ni kuhubiri pale ambapo Yesu alikuwa hajaubiriwa. Rum. 15:20, "*Kadhalika nikijitahidi sana kuihubiri injili, nisihubiri hapo ambapo jina la Kristo limekwisha kutajwa, nisije nikajenga juu ya msingi wa mtu mwingine.*"

Paulo alionyesha kwamba hakuwa haya kwa kupenda kwake na utayari wa kuhubiri muda wowote na sehemu yoyote!

Kwa nini hakuona haya.

Ni uweza wa Mungu uuletao wokovu…

Kwa kila mtu aaminiye, Myunani na wasio Wayunani (Mataifa). Rum. 1:16, "*Kwa maana siionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia.*"

Kwa maana inasema kuhusu Kristo, uwezo wa Mungu na hekima ya Mungu. 1 Kor. 1:23-24, "*Bali sisi tunahubiri Kristo aliyesulibiwa; kwa Wayahudi ni kikwazo na kwa Wayunani ni upuzi; bali kwao waitwao Wayahudi kwa Wayunani, ni Kristo nguvu ya Mungu na hekima ya Mungu.*"

Inafunua haki ya Mungu kaatika wokovu.

Jinsi wenye haki wataishi kwa imani. Rum. 1:17, "*Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani; kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Jinsi Mungu alivyo mwenye haki na anavyowapa haki wale wanaomwamini Yesu. Rum. 3:21-26, "*Lakini sasa haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria; inadhuhudiwa na torati na manabii; ni haki ya Mungu iliyo kwa njia ya imani katika Kristo Yesu kwa wote waaminio. Maana hakuna tofauti; kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu; wanahesabiwa haki bure kwa neema yake kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu; ambaye Mungu amekwisha kumweka awe upatanisho kwa njia ya imani katika damu yake, ili aonyeshe haki yake kwa sababu ya kuziachilia katika ustahinili wa Mungu dhambi zote zilizotangulia kufanywa; apate kuonyesha haki yake wakati huu ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabu haki yeye amwaminiye Yesu.*"

Kwa sababu ya uwezo wake na ujumbe, Paulo hakuona haya kuhubiri injili kwa yeyote aliyekuwa tayari kusikiliza!

Basi, kutoka kwa Paulo tunataka kuangalia sababu kadhaa ni kwa nini…

Hatupaswi kuionea haya injili

Injili inabaki kuwa ni ileile.

Bado ni uwezo wa Mungu kuokoa.

Uwezo wa Mungu huzaa imani mioyoni mwa wale wanaoisikia.

Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Uwezo wa Mungu huzaa matunda ndani yao wanaofahamu kweli.

Kol. 1:5-6, "*Kwa sababu ya tumaini mlilowekewa akiba mbinguni; ambalo habari zake mlizisikia zamani kwa neno la kweli ya injili; iliyofika kwenu kama ilivyo katika ulimwengu wote, na kuzaa matunda na kukua kama inavyokuwa kwenu pia tangu siku mlipoisikia mkaifahamu sana neema ya Mungu katika kweli.*"

Bado inafunua haki ya Mungu katika wokovu.

Jinsi Yesu alivyokufa kwa ajili ya dhambi zetu. 1 Kor. 15:1-4, "*Basi ndugu zangu nawaarifu ile injili niliyowahubiri; ambayo ndiyo mliyoipokea na katika hiyo mnasimama, na kwa hiyo mnaokolewa ikiwa mnayashika sana maneno niliyowahubiri isipokuwa mliamini bure. Kwa maana naliwatolea ninyi hapo mwanzo yale niliyoyapokea mimi mwenyewe, ya kuwa Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanenavyo maandiko; nay a kuwa alizikwa, nay a kuwa alifufuka siku ya tatu kama yanenavyo maandiko;*"

Jinsi tunavyoweza kupata ondoleo la dhambi zetu kwa Yesu kupitia imani, toba, na ubatizo.

- Mdo. 2:36-38, "*Basi nyumba yote ya Isreali na ijue yakini ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyo mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo. walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"
- Mdo. 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini?simama ubatizwe ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake.*"

Kupita kwa wakati hakujadhofisha uwezo na ujumbe wa injili ya Kristo!

Hitaji linabaki kuwa ni lilelile.

Roho zinahitaji wokovu.

Wote wametenda dhambi. Rum. 3:23, "*Maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;*"

Mshahara wa dhambi ni mauti. Rum. 6:23, "*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu.*"

Werevu na wajinga, walioko karibu na mbali.

Yesu bado ni njia pekee ya kwenda kwa Baba. Yohana 14:6, "*Yesu akamwambia, mimi ndimi njia kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba bali kwa njia ya mimi.*"

Kupita kwa nyakati haijatoa leseni kwa hitaji ya kuacha injili ya Kristo!

Kutoka katika mfano wa Paulo, tunaweza kujua nia njema na tabia ya…

Wale ambao hawaionei haya injili

Tunakuwa na hisia ya wajibu…

Kwa Mungu aliyewaokoa.

Je hatuna shukurani kwa kila alichotufanyia Mungu? Hii haiwezi kuathiri jinsi tunavyoishi maisha yetu?

Gal. 2:20, "*Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili,ninao katika imani ya Mwana wa Mungu ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"

Kwa wale waliopotea.

Je hatujali kuhusu hatima yao ya milele wanapaswa kufa katika dhambi?

Je hii haiwezi kutupeleka kwenye jambo fulani? 2 Kor. 5:11, "*Basi tukiijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu lakini tumedhihirishwa katika dhamiri zetu pia.*"

Wale ambao hawaionei haya injili watahisi kuwa na wajibu kama wa Paulo.

Rum.1:14, "*Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa rumi.*"

Watakuwa tayari…

Kushiki injili kadiri wapatapo.

Kinachosemwa hakijulikani, watajifunza (hata kurudia kujifunza).

- 1 Pet. 3:15, "*Mwe tayari siku zote kumjibu mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu.*"
- Heb. 5:12, "*Kwa maana iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita) mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu.*"

Hawatapumzika mpaka watakapopata mfumo, mahitaji, au vifaa, ambapo wanaweza kuwasilisha injili kwa wengine. Alafu watatafuta "mlango ulio wazi" kuwafundisha wengine.

1 Kor. 3:5, "*Basi Apolo ni nani? Na Paulo ni nani? Ni wahudumu ambao kwao mliamini; na kila mtu kama Bwana alivyompa.*"

Kuhubiri injili kadiri wapatapo nafasi.

Wanaweza wasiwe katika nafasi ya kwenda, lakini bado wanaweza kutuma watu.

- Rum. 10: 14-15, "*Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikiaje pasipo mhubiri? Tena wahubirije wasipopelekwa kama ilivyoandikwa ni mizuri kama nini miguu yao wahubirio habari ya mema.*"
- 3 Yohana 1:5-8, "*Mpenzi kazi ile ni yaa uaminifu uwatendeayo hao ndugu na hao wageni nao, waliokusudia upendo wako mbele ya kanisa; utafanya vizuri ukiwasafirisha kama ipasavyo kwa Mungu. Kwa maana kwa ajili ya jina hilo, walitoka wasipokee kitu kwa mataifa. Basi imetupasa sisi kuwakaribisha watu kama hao, ili tuwe watenda kazi pamoja na kweli.*"

Wanaweza wasiwe katika nafasi ya kufundisha, lakini bado wanaweza kukaribisha.

- Mdo. 10:24, "*Siku ya pili yake wakaingia Kaisaria. Na Kornelio alikuwa akiwangojea, hali amekusanya jamaa zake na rafiki zake.*"
- Mdo. 10:33, "*Mara nikatuma watu kwako, nawe umefanya vyema kuja. Basi sasa sisi sote tupo hapa mbele za Mungu tupate kuyasikiliza maneno yote uliyoamriwa na Bwana.*"

Alafu watakuwa wanatazamia "mlango uli wazi" kutuma.

Fil. 4:15-16, "*Nanyi pia, nanyi wenyewe mnajua enyi Wafilipi ya kuwa katika mwanzo wa injili nilipotoka Makedonia hakuna kanisa lingine lililoshirikiana nami katika haabari hii ya kutoa naa kupokea ila ninyi peke yenu. Kwa kuwa hata huko Thesalonike mlinileteaa msaadaa kwa mahitaji yangu, wala si mara moja.*"

Wale wasioionea haya injili watajiweka tayari kama Paulo.

Rum. 1:15, "*Kwa hiyo kwa upande wangu mimi ni tayari kuihubiri injili hata na kwenu ninyi mnaokaa rumi.*"

Hitimisho

Je unaionea haya injili ya Kristo? Unaweza ukawa, kama hauko hivyo…

- Kufanya vyovyote kushiriki injili.
- Kujihusisha na wengine kuhubiri injili.

Huna sababu ya kuona haya; bado ni injili ileile.

- Kwa uwezo wa kuokoa roho za wanadamu.
- Ikifunua haki ya Mungu kuwaokoa wanadamu.

Hatupaswi kuionea haya injili, au ya Yesu mwenyewe.

- Marko 8:38, "*Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu.*"
- 1 Pet. 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya bali amtukuze Mungu katika jina hilo.*"